MASHARTI YA CHAMA

CHAMA CHA USHIRIKA CHA

AKIBA NA

MIKOPO CHA TANESCO

NAMBA YA KUANDIKISHWA: 1843

S. L. P. 9024

SIMU: 2450472

DAR ES SALAAM

TANZANIA

SEHEMU YA KWANZA
JINA LA CHAMA

1. JINA LA CHAMA

a. Jina la Chama litakuwa: **TANESCO SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LIMITED (TANESCO SACCOS).**
b. Anuani ya Chama: S. L. P. 9024, Dar es Salaam, Tanzania.
c. Tarehe ya kuandikishwa: 09 Mei1968.
d. Nambari ya kundikishwa: 1843.
e. Idadi ya Wanachama waliofanya maombi ya kuandikishwa: 10 (kumi).
f. Eneo la shughuli za Chama: TANZANIA BARA.
g. Makao Makuu ya Chama yatakuwa: DAR ES SALAAM.

SEHEMU YA PILI
LENGO NA MADHUMUNI

2. MADHUMUNI YA CHAMA HIKI YATAKUWA

TANESCO SACCOS ni Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa Shirika la Umeme – TANESCO ambao wamejiunga pamoja kwa hiari kwa madhumuni ya kuinua na kustawisha hali ya uchumi na maisha yao kwa kuanzisha na kumiliki TANESCO SACCOS kidemokrasia na kuchangia mtaji na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za Vyama vya Ushirika.

Ili kufikia lengo la kukidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii ya Wanachama, Chama kitafanya yafuatayo:-

a. Kupokea Hisa, Akiba na Amana ya fedha toka kwa Wanachama na kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa Wanachama wake.
b. Kuimarisha mtaji wa Chama.
c. Kuwashauri wafanyakazi wa TANESCO wasio Wanachama kujiunga na Chama.
d. Kuwawezesha Wanachama kutumia na kutunza vizuri fedha kwa manufaa yao kwa:-
    i. Kuwahimiza wanachama kuongeza Mafungu, Akiba, Hisa na Amana zao mara kwa mara.
    ii. Kuhifadhi fedha ya Wanachama katika vyombo vya fedha, kununua dhamana za serikali na kuwekeza katika mashirika mbali mbali baada ya kutekeleza madhumuni muhimu ya Chama na kutoa huduma ya mikopo kwa Wanachama.
    iii. Kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya Wanachama na Taifa kwa ujumla kama itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu wa Wanachama na kuidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

SEHEMU YA TATU
UANACHAMA

3. WANACHAMA

TANESCO SACCOS ni Chama cha hiari na Uanachama uko wazi kwa wafanyakazi wote wa TANESCO na Waajiriwa wa TANESCO SACCOS wenye uwezo wa kutumia huduma zake na walio tayari kukubali wajibu na majukumu ya kuwa Mwanachama bila kubaguliwa kijinsia, kijamii, kisiasa au kidini wanaokubalika baada ya kufuata na kutimiza masharti ya kujiunga na chama.

4. SIFA ZA MUOMBAJI UANACHAMA

a. Mfanyakazi atakayejiunga na chama hiki awe ni wa kuaminika na kufahamika na Wanachama wenzake.
b. Awe mwenye akili timamu. Awe mwenye uwezo wa kulipa kiingilio na kununua hisa na kuchangia akiba zake kila mwezi.

5. TARATIBU ZA KUJIUNGA KATIKA CHAMA

a. Mfanyakazi anayetaka kuwa Mwanachama atapeleka maombi kwenye Bodi ya Chama kwa kujaza fomu maalum ya maombi iliyobandikwa picha ya mwombaji.
b. Ndani ya kipindi cha siku tisini (90) Bodi iwe imeshughulikia ombi/maombi na kutoa jibu la kukubali au kukataa kwa mwombaji/waombaji kuwa Mwanachama.
c. Mwombaji akikubaliwa kujiunga na chama atalipa kiingilio cha TShs. 10,000.00 na kununua hisa zisizo pungua mbili (2) zenye thamani iliyoonyeshwa katika sehemu ya nne (4) ya masharti haya kati ya hisa ishirini (20) za mwanzo anazotakiwa kununua kwa mujibu wa Masharti haya.
d. Sehemu ya hisa zilizobaki ni lazima zilipwe katika kipindi kisichozidi miezi tisa (9) tangu kujiunga kwake. Aidha Mwanachama ataendelea kuchangia akiba zake kila mwezi (mafungu) kwa kiasi kisichopungua TShs. 30,000.00 au kiasi ambacho kitakuwa kimepangwa na wanachama kulingana na wakati.
e. Chama kitakuwa na Daftari la Wanachama lenye maelezo muhimu ya Mwanachama yakihusisha hisa, kiingilio, mafungu yake ya kila mwezi na majina ya warithi, kwa kuandikwa wazi, na kila Mwanachama atatia saini/dole gumba la kulia mbele ya jina lake.

6. HAKI ZA MWANACHAMA

Mwanachama baada ya kulipa kingilio, kununua hisa zisizopungua mbili na kuchangia akiba yake ya kila mwezi, atakuwa na haki zifuatazo:-

a. Kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za chama kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.
b. Kuhudhuria , kushiriki na kutoa maoni yake katika vikao vya tawi.
c. Kupiga na kupigiwa kura
d. Kuchagua mwakilishi na yeye kuchaguliwa kuwa mwakilishi wa tawi.
e. Kuweka na kutoa, Akiba na Amana zake kwa kufuata masharti na taratibu za chama.
f. Kuongeza hisa zake na kufikia kiwango kisichozidi asilimia ishirini (20%) ya thamani ya hisa zote za Wanachama za wakati uliopo.
g. Kupatiwa mkopo kwa kufuata Masharti na utaratibu uliowekwa.
h. Kuwa mdhamini wa mkopo wa Mwanachama mwenzake.

i. Kusikilizwa, kupewa taarifa na kutazama na kusoma masharti, mizania, mihutasari ya mikutano mikuu na nyaraka zote za Chama wakati wa saa za kazi.
j. Kuitisha Mkutano Mkuu Maalum wa Chama kwa kufuata sheria, kanuni na masharti ya Chama.
k. Kupewa hati ya uthibitisho wa kumiliki hisa katika chama baada ya kulipia hisa zote ishirini (20) za mwanzo (Share Certificate).
l. Kushiriki katika kufanya marekebisho ya Masharti ya Chama.
m. Kuacha Uanachama.
n. Mwanachama ambaye uanachama wake umekoma, baada ya kulipa deni lake analodaiwa na Chama, atarejeshewa Hisa, Akiba, Amana na haki zake nyingine ndani ya siku thelathini (30) tangu siku uanachama ulipokoma.
o. Kukata rufaa.
p. Kuchagua mrithi wake.

7. WAJIBU WA MWANACHAMA

Kila mwanachama wa Ushirika huu atawajibika kwa Chama kama ifuatavyo:-

a. Kulipa kiingilio, kununua hisa na kulipa akiba ya kila mwezi kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa. Aidha anatakiwa atoe michango yote anayotakiwa kutoa kama itakavyoamuliwa katika Mkutano Mkuu.
b. Kulipa madeni yote katika chama kwa ukamilifu na kwa wakati unaokubalika.
c. Kubeba (Liability) dhima iwapo janga lolote litatokea. Dhima hiyo kikomo chake ni kiasi cha hisa zake katika Chama.
d. Kuhudhuria vikao vya Chama tawini kila vinapoitishwa na kushiriki kikamilifu katika vikao hivyo na kutekeleza maamuzi ya Mkutano Mkuu.
e. Kuheshimu mikataba ikiwa ni pamoja na kulipa mkopo alioudhamini endapo mkopaji atashindwa kulipa mkopo wake kama alivyoahidi bila sababu za msingi.
f. Kununua hisa pamoja na kuchangia akiba kwa mujibu wa masharti haya, kifungu Na. 5 c. na d.
g. Kuyaelewa masharti ya Chama na kuyafuata pamoja na kuzielewa na kuzifuata sheria na kanuni za vyama vya ushirika, nyaraka za Mrajis wa vyama vya Ushirika na sera za chama.
h. Kudhamini na kutetea Chama pamoja na Wanachama wake pale ambapo hali ambayo haitoi sura nzuri inapojitokeza, kupitia kamati ya usimamizi, Bodi, au kwa mwakilishi wa wanachama kwa maandishi au Mrajis wa vyama vya Ushirika.

8. KUACHISHWA UANACHAMA

Mwanachama anaweza kusimamishwa au kufukuzwa uanachama kutokana na sababu zilizomo Katika Kifungu cha 26(1) cha kanuni za Ushirika za Mwaka 2004 na marekebisho yake.
a. Kuhukumiwa kwa kosa la kutokuwa mwaminifu au kufungwa jela kwa kosa la jinai.
b. Kutoa rushwa kwa viongozi au mtumishi wa Chama kwa nia ya kufanyiwa upendeleo.
c. Kutoa vitisho kwa viongozi na wafanyakazi wa Chama kwa nia ya kufanikisha azma yake.
d. Kufanya kitendo ambacho Bodi ya Chama na Mkutano Mkuu utaridhika kuwa ni cha kutokuwa mwaminifu au ambacho ni kinyume na madhumuni ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.
e. Kushindwa kulipa mkopo kwa muda ulioruhusiwa na Chama bila kuwa na sababu zinazokubalika na Bodi ya Chama.

f. Kutumia mali za chama kwa manufaa yake binafsi

9. KUKOMA UANACHAMA

Uanachama utakoma kwa Sababu zozote zilizomo katika kifungu Na. 25 cha Kanuni za Ushirika za mwaka 2004 na marekebisho yake**.**

a. Kujiuzulu mwenyewe baada ya kutoa taarifa ya siku tisini (90) ya maandishi kwa Bodi ya Chama.
b. Kuachishwa uanachama kwa azimio litakaloungwa mkono na wanachama wasiopungua theluthi mbili (2/3) ya wanachama waliohudhuria katika mkutano mkuu.
c. Kurejeshewa hisa zake zote na kuacha kulipia mafungu yake ya kila mwezi.
d. Kifo.
e. Wazimu uliothibitishwa na Daktari.
f. Kuhama Tanzania.
g. Kukataliwa uanachama na theluthi mbili (2/3) ya Wanachama waliohudhuria katika Mkutano Mkuu baada ya kupewa nafasi ya kujitetea kwa kufanya makosa ambayo yanalazimu kukataliwa na Wanachama.
h. Kukoma kwa ajira

10. KUJIUNGA TENA

Mwanachama aliyejiuzulu, kuachishwa au kufukuzwa Uanachama anaweza kujiunga tena kwa mujibu wa masharti haya ya Chama, baada ya kuonekana kuwa tabia yake imerekebika baada ya miezi sita (6).

11. MRITHI WA MWANACHAMA

Kila mwanachama atamteua mrithi/warithi wake ambao watakuwa na haki ya kulipwa Akiba, Amana na kurejeshewa Hisa na faida. Mwanachama atakuwa na haki ya kubadilisha jina la mrithi/warithi. Kila uteuzi utaandikwa katika daftari ya Wanachama na utatiliwa saini na kuwekwa dole gumba na mwanachama.

SEHEMU YA NNE
HISA ZA CHAMA

12. HISA ZA CHAMA

Hisa ni fedha inayotolewa na Wanachama na kuwa sehemu ya mtaji asilia (“Core Capital”) kwa ajili ya shughuli za Chama.

a. Hisa moja itakuwa na thamani ya TShs. 10,000.00 (elfu kumi).
b. Hakuna mwanachama atakayeruhusiwa kununua hisa zaidi ya asilimia ishirini (20%) ya hisa zote za Chama.
c. Mwanachama anaweza kurejeshewa au kupunguza hisa zake Kwa mujibu wa masharti yafuatayo:-
    i. Mwanachama anayetaka kurejeshewa hisa zake ataelezea nia yake hiyo kwa maandishi na atakuwa na haki ya kurejeshewa ndani ya siku sitini (60) bila kuathiri mtaji wa Chama.

ii. Mwanachama atakayetaka kupunguza hisa zake za ziada bila kuathiri uanachama wake ataelezea nia yake hiyo kwa maandishi na maombi yake kujibiwa ndani ya siku sitini (60) na Bodi ya Chama.

iii. Iwapo mwanachama anadaiwa na Chama, hisa zake zitakuwa moja ya dhamana ya deni.

d. Mwanachama hataweza kuhamisha hisa zake katika chama ila tu kama hisa zake zitakuwa katika Chama kwa muda usiopungua miaka mitano (5) au kama uhamishaji huo utafanywa kwa mtu aliyeomba uanachama na kukataliwa au kama Mwanachama huyo amekosa sifa za uanachama.

e. Mwanachama atakayekuwa na hisa kumi (10) tu au atakayepunguza hisa zake hadi kufikia hisa kumi (10) na iwapo hataongeza kiasi cha hisa hizo kufikia hisa ishirini (20) kwa muda wa miezi tisa (9) ataondolewa kwenye Chama na Uongozi utampa taarifa ya siku thelathini (30) kwa maandishi kwa kutumia anuani yake inayofahamika na Chama.

SEHEMU YA TANO
KUDAIWA KWA CHAMA

13. KUDAIWA KWA CHAMA

a. Dhima (Liability) ya Mwanachama kwa ajili ya madeni ya Chama haitazidi thamani ya hisa zake ambazo hazijalipiwa.

b. Chama kinaweza kukopa baada ya kupata idhini ya Wanachama na Mrajis wa Vyama vya Ushirika:-

i. Kiasi kisichozidi robo (1/4) ya jumla ya hisa zote pamoja na matengo, kwa uamuzi wa angalau robo tatu (3/4) ya wajumbe wa Bodi na kuridhiwa na Kamati ya Usimamizi.

ii. Kiasi zaidi kinaweza kukopwa baada ya kupata uamuzi wa Wanachama ambao watafikiria pendekezo lililofanywa na robo tatu (3/4) ya wajumbe wa Bodi. Lakini kiasi kitakachokopwa kisizidi nusu ya rasilmali ya Chama iliyonayo yaani mtaji, amana na ziada (Capital +Surplus).

SEHEMU YA SITA
MTAJI WA CHAMA

14. MTAJI WA CHAMA

Mtaji wa chama utatokana na:-

a. Hisa na Akiba za wanachama pamoja na ziada ya kila mwaka kwa mujibu wa kanuni za ushirika.

b. Fedha zinazotokana na viingilio na michango maalum au ruzuku

c. Ziada Halisi

d. Akiba ya lazima na malimbikizo mengine

e. Mikopo kutoka vyombo vya fedha, misaada toka kwa wafadhili, Taasisi mbalimbali za umma na nafuu ya kibiashara.

f. Iwapo Mwanachama atakoma uanachama wake kwasababu yoyote ile atatakiwa kuwa amechukua hisa zake Katika kipindi cha Miaka Miwili na iwapo hatazidai yeye au familia yake hisa hizo zitachukuliwa na chama.

SEHEMU YA SABA
UONGOZI NA USIMAMIZI

15. MIKUTANO MIKUU

a) Maamuzi makuu yanayohusu Chama yatakuwa mikononi mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu husika .

b) Wajumbe wa Mkutano Mkuu watakuwa ni:-
   i. Wajumbe wa Bodi
   ii. Wajumbe wa kamati ya usimamizi
   iii. Mwakilishi wa wanachama
   iv. Wawakilishi wa wanachama watakaochaguliwa na wanachama kutoka Makao Makuu ya TANESCO, Mikoa, Wilaya pamoja na Vituo vya kufua Umeme kwa uwiano wa idadi ya wanachama waliopo.

c) Mkutano Mkuu utakuwa na Wajumbe wasiozidi Mia tatu (300)

15.1 MKUTANO MKUU WA MWAKA

1. Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Chama utafanyika mara baada ya kufunga mwaka wa Chama, tarehe 31 Desemba ya kila mwaka na isizidi miezi sita (6) ukichelewa sana.
2. Mambo yafuatayo lazima yajadiliwe katika mkutano mkuu wa mwaka.
   a. Kuthibitisha idadi ya mahudhurio (akidi) kama imetimia kabla ya kuanza mkutano.
   b. Kusoma na kuthibitisha mambo ya mkutano uliopita.
   c. Kujadili taarifa ya Ukaguzi (Audited Report), taarifa ya Ukaguzi ya mrajis, taarifa ya Kamati ya Usimamizi na kukubali au kukataa taarifa ya mwaka ya mahesabu (mizania).
   d. Kujadili taarifa ya utendaji ya Bodi ya Chama.
   e. Namna ya kugawa ziada kwa kuzingatia masharti ya chama, kanuni na Sheria ya vyama vya ushirika na marekebisho yake.
   f. Kuzungumzia mambo yanayohusu maendeleo ya chama na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa Bodi.
   g. Kupanga kiwango cha Honoraria kwa wajumbe wa Bodi na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi.
   h. Kuweka kiwango cha riba na faida juu ya amana.
   i. Kuweka idadi ya hisa na thamani yake.

15.2 MKUTANO MKUU WA KAWAIDA

1 Kunaweza kuwa na mkutano mkuu wa kawaida mmoja ambao utafanyika ndani ya kipindi cha miezi mitatu (3) kabla ya mwaka wa fedha wa chama kumalizika.

2. Mambo yafuatayo yatajadiliwa katika mkutano mkuu wa kawaida;-

a. Kuthibitisha muhtasari wa mkutano uliopita.
b. kuhakiki idadi ya wajumbe wa Bodi
c. Kupitia na kufanya marekebisho ya Masharti ya chama kama ikibidi.
d. Kupokea na kujadili taarifa ya maendeleo kutoka kwenye Bodi ya Chama.
e. Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji kutoka kwenye Bodi ya Chama.

f. Kuidhinisha ununuzi au uuzaji wa mali ya chama kwa ujumla na kutoa mali ya chama inayozidi Milioni kumi(10,000,000.00).
g. Kuidhinisha makisio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha unaofuata.
h. Kuweka ukomo wa madeni chini ya sheria ya Vyama vya Ushirika inayotumika.
i. Kuchagua, kuwaondoa madarakani viongozi na wawakilishi wa Chama kwa mujibu wa Sheria na kanuni za ushirika, waraka wa Mrajis na masharti ya Chama.
j. Kuthibitisha kuingizwa na kufukuzwa wanachama.
k. Kuchagua wajumbe kukiwakilisha Chama katika shughuli za Vyama na Taasisi nyingine zinazohusika na maendeleo ya Chama.
l. Kupitia na kupitisha mikataba iliyoingiwa na Bodi kwa niaba ya Chama.
m. Kuzungumza mambo yote yanayohusu maendeleo ya utekelezaji kwenye Bodi.

15 .3 MKUTANO MKUU MAALUM

a. Kutakuwepo na Mkutano Mkuu maalum wakati wowote iwapo utaitishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika au kwa maombi ya maandishi ya wawakilishi wasiopungua theluthi moja (1/3).
b. Kwa mkutano mkuu maalum ulioombwa na wanachama maombi lazima yataje sababu za kutaka mkutano huo ufanyike na waombaji lazima waweke saini zao na kupeleka kwa Mwenyekiti wa chama na nakala kwa Mrajis wa vyama vya Ushirika.
c. Mkutano mkuu maalum hautazungumzia mambo zaidi ya yale yaliyotakiwa kuzungumziwa katika mkutano huo.
d. Mkutano mkuu maalum unaweza kuitishwa na Bodi au Kamati ya Usimamizi kujadili jambo la dharura.

16. TAARIFA ZA MIKUTANO MIKUU

a. Matangazo ya mikutano mikuu yatabandikwa katika ofisi ya Chama kwenye mbao za matangazo na kwa kutumia taratibu zinazokubalika katika sehemu hiyo. Tangazo hilo litabidi lionyeshe wazi tarehe ya mkutano, saa, mahala pa kufanyia mkutano na mambo (Agenda) ya mkutano.
b. Muda wa matangazo kwa mikutano utakuwa:-
    i. Kwa mkutano mkuu wa mwaka si chini ya siku ishirini na moja (21).
    ii. Kwa mkutano mkuu wa kawaida si chini ya ya siku ishirini na moja.(21)
    iii. Kwa mkutano mkuu maalum si chini ya siku saba (7).
c. Siku tatu kabla ya mkutano kufanyika Bodi ya Chama itatoa tangazo la ziada kuwakumbusha wanachama.
d. Siku kumi na nne kabla ya mkutano mkuu wa Mwaka kufanyika Bodi ya Chama itawasilisha makabrasha ya chama na nyaraka zote kwa wawakilishi zitakazojadiliwa kwenye mkutano mkuu wa Mwaka na Mkutano Mkuu wa kawaida.

17. MAHUDHURIO (AKIDI) KATIKA MIKUTANO MIKUU

a. Mahudhurio katika mikutano mikuu ya chama yasiwe chini ya nusu ya Wajumbe wote au Wajumbe mia moja (100) ukichukulia idadi yoyote iliyo ndogo.
b. Kwa mkutano mkuu wa mwaka na mkutano mkuu wa kawaida, ikiwa idadi ya mahudhurio haitoshi baada ya saa moja ya muda uliopangwa kupita, mkutano utaahirishwa kwa siku saba na mambo yatakayozungumzwa yatakuwa ni yale yale ya mkutano ulioahirishwa. Iwapo mahudhurio hayatatosha tena, mkutano hautafanyika na utafutwa.

c. Kama ikibidi, mkutano mkuu maalum ukaitishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika baada ya mkutano mkuu kufutwa, mkutano huo maalum utafanyika kwa mahudhurio yoyote yale na maazimio yatakayotolewa yatakuwa ni halali.

18. MWENYEKITI WA MIKUTANO MIKUU

a. Mwenyekiti wa Chama ataendesha mikutano yote isipokuwa ule mkutano mkuu maalum ulioitishwa na Mrajis ambapo Mrajis mwenyewe au mtu atakayemteua atakuwa Mwenyekiti.
b. Mwenyekiti akiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataongoza mkutano, na iwapo wote wawili hawapo katika dakika 15 baada ya muda wa kuanza mkutano, mjumbe yeyote kati ya waliohudhuria atachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda na ataongoza mkutano.

19. VIKAO VYA MATAWI

Kutakuwepo na vikao vya Matawi viwili kabla na baada ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa chama kufanyika.

19.1 Kikao cha Maandalizi ya Mkutano Mkuu

a. Kikao hiki kitafanyika mwezi mmoja au miwili kabla ya mkutano mkuu wa mwaka.
b. Kikao hiki kitajadili mambo yafuatayo:-
    i. Kuthibitisha (akidi) mahudhurio
    ii. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano wa tawi uliopita.
    iii. Kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya chama na kutoa maoni ya namna bora ya uendeshaji wa shughuli za chama.
    iv. Kuandaa dondoo za kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu.
    v. Kuchagua wawakilishi ambao watahudhuria Mikutano mikuu ya chama kwa niaba yao. Uchaguzi utaratibiwa na viongozi wa chama.

19.2 Kikao cha Mrejesho

a. Kikao hiki kitafanyika mwezi mmoja au miwili baada ya mkutano mkuu wa mwaka.
b. Kikao hiki kitajadili mambo yafuatayo:-
i. Kuthibitisha (akidi) mahudhurio
    ii. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano wa tawi uliopita.
    iii. kupokea taarifa kutoka kwa wawakilishi juu ya maamuzi mbalimbali yaliyofikiwa na mkutano Mkuu.

20. VIONGOZI WA MATAWI

Matawi ya chama yatakuwa na viongozi wakuu wawili, mwenyekiti na katibu watakaochaguliwa miongoni mwa wawakilishi wa mkutano mkuu katika tawi. Viongozi hao watachaguliwa na wanachama wote katika tawi kwa kupigiwa kura za siri.

20.1 MAJUKUMU YA VIONGOZI WA MATAWI

a. MWENYEKITI WA TAWI

Mwenyekiti wa tawi ni kiongozi mkuu na mwakilishi wa Wanachama wote kwenye tawi. Mwenyekiti atachaguliwa na wanachama wote katika tawi. Ataongoza tawi kwa kipindi cha miaka mitatu (3) isipokuwa anaweza kuachishwa na Wanachama kabla ya kipindi hicho na uchaguzi mwingine kufanyika endapo atakuwa na makosa au anakabiliwa na tuhuma. Atakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Atakuwa msemaji mkuu wa tawi
ii. kuitisha na kuongoza vikao vya tawi
iii. Kuwasilisha taarifa za Mkutano Mkuu wa Chama kwenye tawi
iv.Kufanya kazi nyingine zitakazohitaji kusimamiwa kwa niaba ya Uongozi wa chama.
v.kuwasiliana na Meneja wa Chama kuhusiana na masuala mbalimbali ya chama
vi.kuwasilisha taarifa za utendaji toka matawini ambazo zitajadiliwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka.

b. KATIBU WA TAWI

Katibu wa tawi atakuwa mtendaji mkuu wa tawi. Katibu atachaguliwa na wanachama wote katika tawi. Ataongoza tawi kwa kipindi cha miaka mitatu (3) isipokuwa anaweza kuachishwa na Wanachama kabla ya kipindi hicho na uchaguzi mwingine kufanyika endapo atakuwa na makosa au anakabiliwa na tuhuma. Atakuwa na majukumu yafuatayo:-

i. Kupokea barua zote zinazoingia katika tawi na kuzishughulikia.
ii. Kuwa mwandishi mkuu wa kumbukumbu za vikao vyote vya tawi.
iii. Kutayarisha mihutasari ya vikao vya tawi.
iv. Kuandaa taarifa mbalimbali za tawi.
v. Atasimamia utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu zote za tawi.
vi. Kuitisha vikao baada ya makubaliano na Mwenyekiti wa tawi.
vii. Kuhamasisha wafanyakazi wa TANESCO wasio wanachama kujiunga na chama.
viii. Kufanya kazi nyingine zozote kama itakavyoamriwa na tawi.

c.WAWAKILISHI WA MATAWI

Wawakilishi wa matawi watahudhuria Mikutano mikuu ya Chama na watakuwa na jukumu la kuhamasisha wanachama wapya.

KAZI ZA WAWAKILISHI KATIKA CHAMA

i. Kuendesha Mikutano ya wanachama wanao wawakilisha.
ii. Kupokea na kupeleka maoni ya wanachama wanao wawakilisha katika Mkutano Mkuu wa chama.
iii. Kuhudhuria Mkutano Mkuu wa chama na kushiriki kikamilifu.
iv. Kusimamia utekelezaji wa malengo ya Chama kama yalivyoidhinishwa na Mkutano Mkuu.
v. Kufafanua kwa ufasaha kwa wanachama mabadiliko yaliyofanywa katika Sera, na miongozo mbalimbali ya Chama.
vi. Kupitia, kujadili na kupitisha mpango wa kazi wa Chama wa mwaka.
vii. Kupitia, kujadili na kupitisha bajeti ya Chama ya mwaka.

viii. kuwahudumia wanachama.
ix. Kuhamasisha wafanyakazi wa TANESCO ambao sio wanachama kujiunga na Chama.
x. Kusimamia ujazaji wa fomu za taarifa za mwanachama kwa ajili ya kumbukumbu katika daftari la mwanachama.
xi. Kutoa taarifa katika ofisi ya chama ya mambo mbalimbali yanayotokea katika tawi kwa wakati kwa hatua zaidi.
xii. Kuhakikisha wastaafu waliolipwa hisa zao katika tawi, wanakabidhi 'share certificate' kwa mwakilishi na irudishwe ofisini.

WAJIBU WA WAWAKILISHI

i. Kuwa kiungo katika chama.
ii. Kuwa watetezi wa wanachama na chama.
iii. Kutunza taswira ya chama.
iv. Kuunda timu moja na viongozi wa juu katika utendaji kazi wa chama.
v. Kujenga na kuimarisha mshikamano baina ya wanachama na viongozi wa juu.
vi. Washauri wa viongozi wa chama.
vii. Kuwa mfano bora.
viii. Kuhudhuria mkutano mkuu na usipohudhuria kurejesha nauli uliyopatiwa.
ix. Kujua taratibu zinazotakiwa katika kulipa mafao, madai mbalimbali ya wanachama na wafanyakazi.
x. Kurejesha mabaki ya fedha za masurufu (Imprest) iliyotolewa kuendesha vikao katika ofisi ya Chama.

21. VIONGOZI WA CHAMA

a. Kutakuwepo na Viongozi wa Chama wakuchaguliwa kwa kufuata taratibu zilizoainishwa katika kanuni za Vyama vya Ushirika zitakazokuwepo. Viongozi wa Chama watachaguliwa na wawakilishi katika Mkutano Mkuu. Mkutano Mkuu huo utachagua wajumbe wa Bodi tisa (9), wajumbe watatu (3) wa Kamati ya Usimamizi ambao sio wajumbe wa Bodi na mjumbe mmoja (1) Mwakilishi wa wanachama ambaye pia si mjumbe wa Bodi. Kutakuwa na wajumbe wa Bodi ya chama ambao ndani yake wajumbe watatu watachaguliwa kuunda Kamati ya Mikopo. Itakayochaguliwa na Mkutano mkuu/Bodi.
b. Kutakuwa na kamati ya usimamizi yenye wajumbe watatu watakaochaguliwa na mkutano mkuu.
c. Viongozi wanaweza kuchaguliwa kutoka nchi nzima lakini theluthi mbili (2/3) watatoka makao makuu ya Chama.
d. Wawakilishi wa matawi yaliyo nje ya Makao Makuu ya Chama wanaweza kuchaguliwa katika Bodi ya chama, kamati ya usimamizi ila wasizidi theluthi moja (1/3) ya viongozi wote.
e. Viongozi ambao kazi zao zinahusisha utendaji wa kila siku wa chama (Mwenyekiti wa Bodi, Makamu mwenyekiti wa Bodi, Mwenyekiti na katibu wa kamati ya usimamizi pamoja na wajumbe wa kamati ya mikopo) watatoka makao makuu ya chama.

f. Kutakuwa na mwakilishi wa wanachama atakayechaguliwa katika mkutano mkuu wa chama wa mwaka. Mwakilishi wa wanachama atachaguliwa kutoka Makao Makuu ya Chama.
g. Mwakilishi wa wanachama akihamishwa toka makao makuu ya chama atapoteza nafasi yake ya uwakilishi.
h. Kwa kuzingatia kifungu 21(c) cha masharti haya, iwapo kiongozi atahamishwa kutoka makao makuu ya chama na iwapo kuhama kwake kuna athiri kifungu 21 (d) cha masharti atapoteza nafasi yake ya uongozi.

22. MAJUKUMU YA BODI

i. Bodi ambayo itakuwa na idadi ya wajumbe tisa (9) itajumuisha Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti
ii. Wajumbe wa Bodi waliochaguliwa watashika madaraka kwa kipindi kisichozidi miaka tisa (9) mfululizo.
iii. Hakuna mjumbe wa Bodi atakayekuwa madarakani kwa vipindi zaidi ya vitatu vya miaka mitatu mitatu (3).
iv. Mjumbe wa Bodi ataacha madaraka kwa kujiuzulu kwa maandishi, kufukuzwa na Mkutano Mkuu, au kwa mujibu wa Kanuni za Vyama vya Ushirika zitakazokuwepo chini ya sheria ya Vyama vya Ushirika na marekebisho yake.
v. Bodi itafanya mikutano mara moja kila mwezi,ili kuthibiti mzunguko wa fedha ambao ni mkubwa, unaotokana na mtaji wa chama kukua kila mwezi, pia kutokana na mahitaji ya kujadili taarifa za matawi yote nchini.
vi. Mjumbe wa Bodi atakayeshindwa kuhudhuria vikao vinne mfululizo bila sababu inayokubalika na Bodi, ataachishwa uongozi na Bodi itateua mwanachama mwingine badala yake hadi mkutano mkuu unaofuata.
vii. Zitokeapo nafasi katika Bodi,zitatolewa fomu kwa wawakilishi ili waombe nafasi zilizo wazi. Nafasi hizo zitajazwa katika mkutano mkuu unaofuata..

viii. Muhtasari wa majadiliano na maazimio yote ya vikao vya Bodi yaandikwe katika kitabu cha kumbukumbu za vikao na kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu baada ya kuthibitishwa na wajumbe waliohudhuria.
ix. Bodi itafanya shughuli zake zote kwa kushauriana mara kwa mara na Mrajis wa Vyama vya Ushirika au mwakilishi wake.

23. KAZI ZA BODI

a. Bodi itakuwa na jukumu la kusimamia shughuli zote za utendaji za Chama na kuhakikisha taarifa zilizokamilika na sahihi za fedha zinatayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika itakayokuwepo na kuweka udhibiti bora wa ndani wa kulinda mali za Wanachama. Aidha Bodi itahakikisha Wanachama wanapata na kuielewa elimu ya ushirika.
b. Bodi itakuwa na wajibu wa kufanya mambo yafuatayo:-
   i. Kutengeneza sera za Chama.
   ii. Kutafsiri na kutekeleza sera ya maendeleo ya Vyama vya Ushirika.
   iii. Kuhakikisha shughuli za Chama zinaenda kulingana na sheria na kanuni za Vyama vya Ushirika na masharti ya Chama kwa kufuata maadili ya kibiashara.
   iv. Kuhakikisha Chama kinatunza kwa usahihi mahesabu ya Chama kuhusiana na fedha, mali, madeni na matumizi.

v. Kutunza daftari la Wanachama.
vi. Kuhakikisha wakopaji wanalipa madeni yao kama walivyoahidi na kuwachukulia hatua za kisheria wakopaji wasio waaminifu na kupendekeza kwa Wanachama katika mkutano mkuu ufutaji wa mikopo mibaya (madeni mabaya) ambayo haiwezekani kulipwa kabisa.
vii. Kuandaa agenda zote za mikutano na kutekeleza maazimio ya mikutano mikuu na yale ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.
viii. Kupokea na kufikiria maombi ya wanachama wapya na kutoa taarifa ya Wanachama wapya waliokubaliwa katika mkutano mkuu wa mwaka.
ix. Kuweka taratibu za uendeshaji wa shughuli za Akiba na Mikopo.
x. Kusimamia mapato na matumizi yote ya chama na kuhakikisha mikopo inatolewa kulingana na masharti ya utoaji mikopo yaliyowekwa na Bodi ya Chama, isipokuwa kazi ya kuidhinisha maombi ya mikopo.
xi. Kuajiri, kusimamisha, kuachisha au kufukuza kazi watumishi wa Chama kwa kuzingatia sheria za ajira za Chama na Nchi.
xii. Kusimamisha uanachama Mwanachama au Mjumbe yeyote wa Bodi, kutokana na tabia mbaya au kushindwa kutimiza wajibu wake wa kazi na kupeleka mapendekezo katika mkutano mkuu unaofuata ili uamuzi wa mwisho utolewe.
xiii. Katika kuendesha shughuli za chama, Bodi itatumia busara kama wafanyabiashara wa kawaida. Hasara yeyote itakayotokea chamani kutokana na Bodi kutojali wajibu wao na madaraka waliyopewa na Wanachama itawalazimu kufidia hasara hiyo kama itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.
xiv. Kusimamia uandikaji na utunzaji wa vitabu vya mahesabu na kumbukumbu nyingine za fedha.Kupokea taarifa za kazi kutoka kwa Meneja na Mhasibu wa Chama na kuzifanyia tathmini.
xv. Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama itakavyoamriwa na mkutano mkuu.

24. KAMATI YA MIKOPO

a. Kutakuwa na Kamati ya Mikopo ambayo itachaguliwa na Mkutano Mkuu/Bodi.
b. Idadi ya wajumbe wa Kamati ya Mikopo itakuwa ni watatu (3) ambao watachaguliwa na wawakilishi/Bodi.
c. Wajumbe wa Kamati ya Mikopo watakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu, isipokuwa mjumbe anaposimamishwa au kufukuzwa kwa mujibu wa Masharti haya.
d. Mwenyekiti wa kamati ya mikopo atachaguliwa na mkutano mkuu/Bodi.
e. Kamati ya Mikopo itafanya kikao mara moja kila mwezi na vikao vya dharura kama vile ambavyo shughuli za chama zitahitaji Taarifa za vikao hivyo zitatolewa kwa Bodi. Idadi ya juu ya jumla ya wanakamati wote itatosha kuendesha shughuli katika kikao.
f. Mikopo ya maendeleo, elimu, ujasiriamali na ile ya viongozi itaidhinishwa na kushughulikiwa na Kamati ya Mikopo. Rufaa zote za wanachama kuhusu mikopo zitajadiliwa katika vikao vya Bodi na maamuzi kupelekwa kwenye Kamati ya Mikopo kwa utekelezaji.
g. Mikopo ya dharura na matangulizi ya mishahara (Salary advance) itashughulikiwa na Afisa/Maafisa Mikopo.
h. Hakuna mtu yeyote atakayekuwa na mamlaka ya kulipa kutoka katika mfuko wa Chama hiki mkopo usioidhinishwa na Kamati ya Mikopo, Afisa Mikopo au kwa kibali maalum cha azimio la kikao halali cha Bodi ya chama.

25. KAZI ZA KAMATI YA MIKOPO

a. Kamati itafanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni, masharti ya chama na sera za mikopo zilizopo.
b. Kamati ya Mikopo itachunguza kwa uangalifu tabia na hali ya fedha ya kila mwombaji wa mkopo pamoja na dhamana kama zipo, na kuhakikisha uwezo wa kulipwa deni kwa ukamilifu katika muda uliowekwa na kuhakikisha kwamba mkopo unaotafutwa ni wa busara na utaleta manufaa kwa mkopaji. Kamati ya Mikopo itajitahidi iwezekanavyo kusaidia wakopaji katika kuondoa matatizo yao ya kifedha.
c. Kamati ya Mikopo itatengeneza na kuweka kumbukumbu sahihi za mambo yote yatakayofanyika na kamati. Nakala za kumbukumbu hizo ziwe tayari ndani ya siku tatu tangu kufanyika kwa shughuli hizo, na kuzituma kwa mwenyekiti wa Bodi na kamati ya Usimamizi.
d. Kamati ya mikopo itatunza daftari la kumbukumbu za vikao vyake vya kila mwezi.
e. Kufanya kazi nyingine zozote kama itakavyoamriwa na Bodi.

26.MWENYEKITI WA CHAMA

Mwenyekiti wa Chama ni kiongozi mkuu na mwakilishi wa Wanachama wote. Mwenyekiti atachaguliwa na Mkutano Mkuu. Ataongoza chama kwa kipindi cha miaka mitatu (3) isipokuwa anaweza kuachishwa na wawakilishi kabla ya kipindi hicho na uchaguzi mwingine kufanyika endapo atakuwa na makosa au anakabiliwa na tuhuma.

27. WAJIBU NA KAZI ZAKE

a. Kuongoza mikutano yote mikuu ya Chama isipokuwa mikutano mikuu maalum
b. kuongoza vikao vya Bodi ya Chama.
c. Msemaji mkuu wa Chama.
d. Kutoa taarifa za maendeleo ya Chama katika Mkutano Mkuu wa Chama.
e. Kutia saini hati za mikatabakwa idhini ya mkutano mkuu wa chama new,
f. Kutia saini mihutasari ya Chama na nyaraka nyingine kwa niaba ya Chama.
g. Kuwasiliana na Kamati ya Usimamizi mara kwa mara.
h. Kuongoza kazi nyingine zitakazohitaji kusimamiwa na Mwenyekiti kadri itakavyoamuriwa na Bodi au Mrajis wa vyama vya ushirika.

28. MAKAMU MWENYEKITI WA CHAMA

Makamu Mwenyekiti atachaguliwa katika Mkutano Mkuu na atashika madaraka kwa muda wa miaka mitatu (3), isipokuwa anaweza kusimamishwa au kuachishwa wadhifa wake na Wanachama kwenye mkutano mkuu kabla ya kipindi hicho.

29. KAZI ZAKE

a. Kusimamia mikutano yote ya Bodi na Wanachama endapo Mwenyekiti hayupo.
b. Kuwa msaidizi wa Mwenyekiti.
c. Kuwa mratibu wa Elimu na Mafunzo.

30. MENEJA WA CHAMA

Kutakuwepo Meneja ambaye ni mfanyakazi wa chama.

31. KAZI ZA MENEJA/KATIBU WA CHAMA

a. Meneja wa chama ndiye atakuwa kiongozi mkuu wa ofisi na shughuli za chama.
b. Kupokea barua zote zinazoingia na kuzishughulikia.
c. Kuwa mwandishi mkuu wa kumbukumbu za vikao vyote vya Bodi na Mikutano Mkuu ya chama.
d. Kutayarisha mihutasari ya vikao vya Bodi na ile ya mikutano mikuu.
e. Atasimamia utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu zote za Chama, isipokuwa Mkataba wake wa ajira na taarifa zinazomuhusu.
f. Kutia saini kwenye hati za malipo
g. Atasimamia watumishi wote wa chama.
h. Kuitisha mikutano/vikao baada ya makubaliano na Mwenyekiti wa Bodi.
i. Kufanya kazi nyingine zozote kama itakavyoamriwa na Bodi.

32. KAMATI YA USIMAMIZI

Kutakuwa na Kamati ya Usimamizi ya Chama yenye wajumbe watatu (3) ambao sio wajumbe wa Bodi. Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi watachaguliwa na wawakilishi katika Mkutano Mkuu wa mwaka.

a. Wajumbe wa kamati hii watashika madaraka yao kwa muda wa miaka tisa na mjumbe mmoja ataondolewa kwa kupigiwa kura na wajumbe wa mkutano mkuu na nafasi yake kujazwa na mwanachama mwingine kwa kupigiwa kura kila baada ya miaka mitatu.
b. Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi anaweza kuacha madaraka kwa kujiuzulu kwa maandishi au kufukuzwa na Mkutano Mkuu wa mwaka.
c. Kamati ya Usimamizi itafanya kikao mara moja kwa mwezi kujadili na kuhakiki kazi za chama na vikao vya dharura inapolazimu kufanya hivyo.
d. Itokeapo nafasi katika Kamati ya Usimamizi,zitatolewa fomu kwa wawakilishi kwa ajili ya kuomba nafasi hizo kwenye mkutano mkuu unaofuata. wajumbe wa kamati ya usimamizi pamoja na Bodi watakaa pamoja kwa ajili ya kupendekeza na kuchagua majina ya wanachama wa kujaza nafasi hiyo kwa kuwapigia kura.
e. Kamati ya Usimamizi haitashiriki moja kwa moja katika kazi za za kuendesha shughuli za chama.
f. Kazi ya Katibu na Mwenyekiti inaweza kushikwa na mjumbe mmoja .

33. KAZI NA MAJUKUMU YA KAMATI YA USIMAMIZI

Kamati ya Usimamizi itachaguliwa na wawakilishi na itawajibika kwa Wanachama kwa kutoa taarifa huru. Kwa mantiki hiyo, Kamati hii itakuwa na kazi zifuatazo:-

a. Kuhakikisha kuwa ukaguzi wa Hesabu za chama unafanyika kila mwaka.
b. Kuwasilisha taarifa ya kamati ya usimamizi wa shughuli za chama kwenye mkutano mkuu wa mwaka kwa wawakilishi.
c. Kuhakiki salio la akiba na baki za mikopo ya Wanachama.
d. Kudumisha mahusiano ya siri na Wanachama.
e. Kupitia taarifa za hesabu za wakaguzi wa ndani wa chama.
f. Inapolazimu kuitisha mkutano maalum.
g. Kuhakiki vitabu vya mahesabu za chama (book of accounts) na kumbukumbu nyingine zikiwemo vitabu vya akiba vya wanachama (Passbooks) na kuhakikisha rejesta za chama zinajazwa na kutunzwa kwa usahihi na uangalifu.

h. Kufuatilia utekelezaji wa maazimio yaliyotolewa pamoja na maoni ya wanachama kwenye mkutano mkuu wa mwaka.

34. MWAKILISHI WA WANACHAMA.

Mwakilishi wa wanachama atachaguliwa na wawakilishi katika Mkutano mkuu na atawajibika kwa wanachama. Mwakilishi wa wanachama atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu (3) tu na mkutano mkuu utakuwa na mamlaka ya kuchagua Mwakilishi mwingine.

Mwakilishi wa wanachama anaweza kusimamishwa na kikao cha pamoja cha Bodi na kamati ua Usimamizi kwa sababu za kushindwa kutekeleza majukumu yake na nafasi yake kushikwa na mwanachama aliyeshika nafasi ya pili wakati wa uchaguzi. Taarifa ya kusimamishwa kwake itapelekwa katika Mkutano mkuu unaofuata kwa ajili ya maamuzi ya mwisho.

35. KAZI NA MAJUKUMU YA MWAKILISHI WA WANACHAMA.

a. Mwakilishi wa wanachama atahudhuria mikutano ya nje itakayohusisha chama.
b. Kuwasilisha taarifa za wanachama wanaohitaji msaada wa Chama katika Bodi kwa uamuzi.
c. Kuratibu kazi na mawasiliano na wawakilishi wa wanachama mikoani.
d. Mwakilishi anaweza kualikwa katika vikao vya Bodi.

SEHEMU YA NANE

TARATIBU ZA KUWEKA AKIBA

36. TARATIBU ZA KUWEKA AKIBA

a. Kila Mwanachama atakayejiunga na Chama atapatiwa Kitabu cha Akiba (“Pass Book”) ambacho kitaonyesha kiasi cha Akiba, Hisa, na Amana alizonazo. Aidha kitaonyesha mikopo na baki ya hisa, akiba, amana na mkopo ambao haujarejeshwa.
b. Vitabu vya akiba vitawekwa nambari zinazofuatana na mara moja kutolewa kwa Mwanachama. Nambari ya vitabu hivi iandikwe kwenye daftari ya Wanachama na katika kadi yake ya akiba na mikopo.
c. Fedha yote ya Wanachama inayopokelewa chamani iingizwe kwenye safu ya kitabu inayohusika na kuwekwa saini na Mhasibu au mfanyakazi mwingine aliyeidhinishwa kupokea fedha kisha kitabu hicho apewe Mwanachama kikiwa kama stakabadhi yake rasmi kwa kumbukumbu ya shughuli zote za baadaye.
d. Kitabu cha Akiba kitatunzwa na Mwanachama mwenyewe. Kitabu kikipotea na upotevu huo ukithibitishwa na Bodi kitabu kingine kitatolewa na Mwanachama atalazimika kulipa ada ya kiasi kilichowekwa na Bodi.
e. Kitabu cha Akiba kionyeshwe wakati wote wa kuweka fedha na wakati wa kuchukua mkopo ili mhasibu aweze kuingiza kiasi kilichowekwa au kinachokopwa.
f. Fedha zitakazowekwa chamani zitaletwa na Mwanachama kwa njia moja wapo kati ya njia zifuatazo au zote:-

i. Makato kutoka kwenye mshahara wa Mwanachama na kuwasilishwa na mwajiri kwa Mhasibu wa chama.
ii. Kupeleka fedha taslim au hundi kwenye akaunti ya chama.

SEHEMU YA TISA
TARATIBU ZA UTOAJI MIKOPO

37. TARATIBU ZA UTOAJI MIKOPO

Utaratibu wa utoaji Mikopo yote utabaki kama ulivyoelezwa kwenye Sera ya Mikopo na kufanyiwa marekebisho pale itakavyohitajika kufanywa hivyo.

SEHEMU YA KUMI
MGAO WA ZIADA

38. MGAO WA ZIADA

Mgao wa ziada utafanyika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika zitakazokuwepo.

a. Kila mwaka Chama kitatenga kiasi cha asilimia ishirini (20%) kutokana na faida halisi kwa ajili ya akiba ya lazima ("Statutory Reserve Fund").
b. Kitatenga asilimia kumi (10%) ya faida halisi kwenye mfuko wa kukombolea hisa za wanachama ("Share Transfer Fund") walioacha uanachama lakini kiasi cha mfuko huo hakitazidi asilimia kumi (10%) ya mtaji halisi wa Chama ("Core capital = member shares+20% retained net earnings every year+10% of total savings every year").
c. Asilimia kumi na tano (15%) ya faida halisi itawekwa kwenye mfuko wa madeni mabaya lakini mfuko huo usiwe na kiasi zaidi ya asilimia kumi na tano(15%) ya madeni yote.
d. Akiba ya lazima itabakia kuwa ni mali ya Chama hiki na haitaweza kugawanywa isipokuwa kama Chama kimevunjwa.
e. Bodi inaweza kupendekeza kwa Mkutano Mkuu kuongeza mifuko mingine iwapo Chama kina mapato halisi ya kutosha.
f. Baada ya matengo ya lazima kutolewa, ziada itagawiwa kwa mujibu wa kifungu (67) (d) cha kanuni za ushirika za mwaka 2004 na marekebisho yake.
g. Hisa zitakazostahili kulipwa faida ni zile zilizokamilika katika kipindi cha miezi kumi na mbili (12).

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
KANUNI ZA FEDHA

39. UHASIBU

a. Chama kitafuata mtindo wa uhasibu katika kutunza vitabu vya Hesabu kwa kufuata viwango vya kimataifa (IFRS) na kanuni za fedha (Financial regulations) zilizopitishwa na Bodi ya chama.
b. Mwaka wa fedha wa Chama utaanza tarehe 01 Januari hadi tarehe 31 Desemba ya kila mwaka.
c. Fedha za Chama hiki zitahifadhiwa katika benki.

d. Mahitaji ya mikopo ya wanachama yakishatoshelezwa, fedha za ziada zinaweza kuwekwa Benki kwenye akaunti za akiba za muda mrefu ili zipate faida.
e. Malipo yote yalipwe kwa Hundi.
f. Fedha ambayo haitumiki kwa mikopo ya wanachama inaweza kuwekwa/kuwekezwa katika:-
    i. Benki itakayopendekezwa kwenye kikao halali cha Bodi
    ii. Kununua hisa katika mabenki na Vyama vya Ushirika ambavyo vimeandikishwa serikalini.
    iii. Shirika lolote lenye mamlaka ya kuhifadhi akiba ya fedha au dhamana za umma.
    iv. Mikopo na hisa za Vyama vingine vya akiba na mikopo.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
KANUNI NA MUUNDO WA UTUMISHI

40. MAMLAKA YA KUAJIRI

Mamlaka ya kuajiri wafanyakazi yatakuwa chini ya Bodi ya Chama kwa mujibu wa masharti haya.

41. AINA YA AJIRA

Bodi ya chama itakuwa na mamlaka ya kuamua aina ya ajira zitakazotangazwa kulingana na mahitaji ya wakati husika, na hivyo kurekebisha kanuni husika za ajira.

SEHEMU YA KUMI NA TATU
MENGINEYO

42. MIGONGANO YA KIMASLAHI

Hakuna mjumbe wa Bodi na mjumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Chama hiki, afisa, wakili au mfanyakazi yeyote wa Chama hiki atakaye jiidhinishia au kujiamulia mwenyewe kuzipata fedha za Chama zinazohusu yeye binafsi au shirika au kampuni au chama kingine ambamo anahusika kwa namna yeyote ile.

a. Mjumbe wa Bodi akiwa na mahusiano na mfanyakazi anayetarajiwa kuajiriwa na chama ni lazima aweke wazi/bayana mahusiano yake na mwajiriwa kwa wajumbe wa Bodi na hatahusika katika mchakato wa ajira.

b. Viongozi na watendaji wa Chama hawataruhusiwa kufanya biashara na chama ili kuepusha migongano ya kimaslahi.

43. NYARAKA ZA CHAMA

Vitabu vya Hesabu na kumbukumbu nyingine za Chama hiki zinaweza kuchunguzwa wakati wowote na Mwanachama yoyote yule.

44. SIRI ZA CHAMA

Wajumbe wa Bodi na kamati ya usimamizi,mwakilishi wa wanachama na watumishi wa chama watatunza siri kuhusu kumbukumbu za Wanachama binafsi isipokuwa masuala ya utoaji na

ukusanyaji wa mikopo ambayo Bodi inaweza kuchukua hatua zozote za lazima dhidi ya wakopaji wasiokuwa waaminifu.

45. HONORARIA KWA WAJUMBE WA BODI / KAMATI YA USIMAMIZI.

Kila mwisho wa mwaka wa fedha kiasi fulani cha faida halisi kitatolewa kwa idhini ya Mkutano Mkuu kama tuzo kwa viongozi wa Chama kwa kazi ya kuridhisha waliyofanya lakini tuzo haiwezi kutolewa iwapo watu hao wameajiriwa na Chama na wanalipwa mshahara, na iwapo Chama kitakuwa hakikutengeneza faida.

46. UTATUZI WA MIGOGORO AU MALALAMIKO

a) Migogoro au malalamiko yeyote kuhusu Masharti au huduma za Chama yatafuata utaratibu wa Vyama vya Ushirika.
b) Sanduku la maoni litawekwa katika ofisi za chama kwa ajili ya kupokea malalamiko mapendekezo na ushauri kutoka kwa wanachama na litafunguliwa mara mbili kwa mwezi.
c) Funguo za sanduku la maoni zitatunzwa na mjumbe mmoja wa kamati ya usimamizi na mjumbe wa Bodi atakayeteuliwa.

47. MAREKEBISHO YA MASHARTI

Masharti haya yanaweza kurekebishwa kwa maamuzi ya Wanachama katika Mkutano Mkuu.

48. UENDESHAJI WA KAZI

Bodi inaweza kutunga sera na kanuni ndogondogo kwa namna itakavyoona inafaa katika kuendesha kazi za Chama. Sera zote ndogondogo zitakazotungwa zitaandikwa katika kitabu cha kumbukumbu na kutangazwa kwa wahusika na kuwekwa kwenye mbao za matangazo.

49. SERA ZA CHAMA

Sera ni mwongozo uliowekwa au kuandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa jambo au shughuli ya Chama. Kwa mujibu wa Masharti haya, Bodi inao uwezo wa kuunda sera mbalimbali za chama zinazohusu mikopo, amana, akiba nk ambazo zitatumika baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa mwaka.

50. MIIKO YA UONGOZI ("CODE OF CONDUCT")

1) Miiko ya uongozi wa Chama hiki itafuata kifungu cha miiko ya uongozi wa vyama vya ushirika kama kitakavyokuwa kimeandikwa katika Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika zitakazokuwepo.
2) Tabia na mwenendo wa viongozi wa SACCOS ya TANESCO vimeainishwa katika kanuni na maadili ya wafanyakazi na viongozi wa Chama ambapo toleo la kwanza lilitoka mwaka 2006.

51. RAMBIRAMBI

1. Kutakuwa na mfuko wa rambirambi ambao kila mwanachama atachangia mara moja kiasi cha Tshs. 10,000/= kutoka katika mshahara wake.
2. Fedha za mfuko wa rambirambi zitakopeshwa kwa wanachama na faida itasaidia kutunisha mfuko huu.
3. Maamuzi ya mwisho ya matumizi ya mfuko huu yatafanywa na wanachama wenyewe.

52. UFAFANUZI

Maneno yafuatayo yanapotumika katika masharti haya yatakuwa na maana kama inavyoelezwa hapa:-

1. Kiongozi - Ina maana ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mwakilishi wa wanachama na Wajumbe wote wa Bodi na Kamati ya Usimamizi pamoja na Meneja Chama.
2. Mrajis - (Registrar of Cooperative Societies) ina maana Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara.
3. Afisa - Ina maana mtu aliyeteuliwa kuidhinisha mikopo maalum.
4. Savings and Credit Cooperative Society - Ina maana Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo (SACCOS).
5. Mikopo Maalum maana yake ni mikopo ya dharura na mkopo wa papo kwa papo (Salary Advance).
6. Makao makuu ya chama- ina maana Mkoa wa Dar es Salaam.

SEHEMU YA KUMI NA NNE
KUFUTWA KWA CHAMA

53. KUFUTWA KWA CHAMA

a. Chama hiki kinaweza kufutwa katika daftari la Vyama vya Ushirika chini ya kifungu cha kufutwa kwa Chama Cha Ushirika kama kitakavyokuwa kimeandikwa katika Sheria ya Vyama vya Ushirika itakayokuwa inatumika.
b. Chama hiki kinaweza kuvunjwa kutokana na Azimio la robo tatu (3/4) ya Wawakilishi wote katika Mkutano Mkuu.
c. Kama idadi ya Wanachama itapungua na kubaki chini ya ishirini (20).

54. MAJINA YA WADHAMINI KUMI (10) WALIOTIA SAINI ZAO KWA NIABA YA WANACHAMA WENZAO

Sisi tulioorodheshwa majina yetu na kusaini hapa chini, tunathibitisha kwa niaba ya Wanachama wote wa TANESCO SACCOS ya kwamba marekebisho ya Masharti haya yamepitishwa kwa kuungwa mkono na Wanachama katika Agenda Na. II na Azimio la Mkutano Mkuu wa Mwaka wa TANESCO SACCOS uliofanyika tarehe 30 Desemba 2012 katika ukumbi wa nje wa mikutano wa NSSF WATER FRONT jijini Dar es Salaam, Tanzania.

Na.	Jina la Mwanachama	Saini
1	ALLY A. MWANANA	
2	PETER D. MWAIMU	
3	MWANDU MASABENDE	
4	THOMAS F. SAMO	
5	SOMOE I. NGUHWE	

6	JOSELINE E. ANYANDWILE	
7	MONICA P. KOMBA	
8	JOHN B. MTEGA	
9	JOHN P. MWASOMBA	
10	MARTHA P. NYALUSI	